

## Maswali

1. Yesu na wanafunzi wake walikuwa wanaenda wapi?
2. Yesu alituma nani kijijini?
3. Yesu aliwambia wafanye nini?
4. Watu wawili waliwaliza wanafunzi nini?
5. Wanafunzi walijibu nini?
6. Wanafunzi waliweka nini juu ya punda?
7. Nani walikuja kumlaki Yesu?
8. Watu walipaza sauti eti nini?
9. Watu walipeperusha nini?
10. Nani mfalme mkuu aliyejkuwa anakuja Yerusalemu?

## Majibu

1. Walikuwa wanaenda Yerusalemu.
2. Yesu alituma wanafunzi wawili kijijini.
3. Aliwambia walete punda.
4. Watu waliwaliza "Mbona mnamchukua punda?"
5. Wanafunzi walijibu, "Bwana Yesu anamtaka."
6. Wanafunzi waliweka nguo zao juu ya punda.
7. Umati wa watu ulikuja kuwalaki.
8. Watu walipaza sauti, "Hosana! Amebarikiwa ajaaye kwa jina la Bwana."
9. Watu walipeperusha matawi ya mitende.
10. Yesu ndiye Mfalme Mkuu aliyejkuwa akija Yerusalemu.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

# 44 Yesu anaingia Yerusalemu

## Marejeo

Mathayo 21: 1—11

## Kiini cha somo

Kuonyesha furaha iletwayo na Yesu


## Maneno maalum

1. Yesu + wanafunzi wawili + leta punda + wanafunzi wanapata punda + ya Yesu.
2. Nguo + Yesu alipanda + watu wanamkaribisha + matawi ya mitende + Hosanna.
3. Yesu + Yerusalemu + furaha + mfalme mkuu.

**44.1** Wakati Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wanakwenda kuingia Yerusalem, mji mkuu. Njiani walifika katika kijiji kidogo. Yesu akawaita wanafunzi wake wawili akawaambia, "Enendeni mpaka kijiji kile kinachowakabili na mtamwona punda akiwa amefungwa kando ya barabara, mfungueni, mnilettee."


Wanafunzi wale wawili wakaenda haraka mara moja. Na walipoingia katika kijiji kile, walimkuta punda akiwa amefungwa kando ya barabara, kama Yesu alivyokuwa amewaambia. Wakamfungua na kumwongoza njiani. Watu wawili waliokuwa wamesimama pembeni waliwaliza, "Kwa nini mnamfungua punda?"

Na Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi jinsi ya kuwajibu ikiwa mtu yeyote angewauliza, Kwa hiyo wakajibu, "Bwana Yesu anahaja naye," na kama Yesu alivyokuwa amewaambia waseme, basi wale watu wakawaruhusu wanafunzi wamchukue yule punda.



**44.2** Yule punda hakuwa na tandiko juu yake, hivyo badhi ya wanafunzi wakatandika nguo zao juu yake, na Yesu akakaa juu yake na kumwongoza yule mwanapunda kuelekea Yerusalem. Na alipokaribia kuingia mjini, watu wengi wakatoka mjini ili kumlaki Yesu. Walipomwona Yesu akiwa amepanda mwanapunda kama vile Mfalme, walifurahi sana. Watu wakavunja matawi ya mitende ndipo wakaanza kushangilia kwa furaha. Wakawa wakimzunguka Yesu huku wakishangilia na kusema, "Hosana, Ndiye mbarikiwa, Mfalme ajaye kwa jina la Bwana"

Mkutano uliendelea kuongeza idadi ya watu sana, watu wengi wakazidi kuongezeka walipokuwa wakisikia kelele za furaha na kuimba nyimbo. Watu wakatupa nguo zao barabarani ili Yesu apite juu yake kana kwamba ni zulia kubwa lililokunjuliwa katika barabara yote. Ilikuwa ni siku iliyo kuu. Na kila mtu alikuwa na furaha kwa jinsi walivyokuwa wakipaza sauti za furaha, "Hosana, Ndiye mbarikiwa, Mfalme ajaye kwa jina la Bwana."



**44.3** Na hatimaye, Yesu akaingia Yerusalem. Matawi ya mitende yaliinuliwa juu, nguo zenye rangi tofauti zilitandazwa kama zulia, wanaume, wanawake na watoto waliimba nyimbo na zaburi. Kila mtu alikuwa ni mwenye furaha na kumshangilia Yesu Mfalme mkuu amekuja Yerusalem.